# MWONGOZO WA UTARATIBU WA KUTOA ULINZI WA KIMATAIFA KATIKA NCHI YA AYALANDI




www.unhcr.ie

UNHCR
The UN Refugee Agency

# Kutuhusu

Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa ya Wakimbizi ni wakala wa Umoja wa Mataifa ambao umepewa mamlaka ya kuwalinda watu waliolazimika kutoroka kwao na kupata usalama katika nchi nyingine. Ofisi ya kitaifa ya UNHCR Ayalandi inafanya kazi ili kulinda haki na hali njema ya wakimbizi, watafutaji hifadhi ya wakimbizi na watu wasio na taifa nchini Ayalandi kupitia kutoamwongozo, mafunzo na usaidizi kwa mamlaka husika na kuimarisha viwango bora zaidi vya kimataifa katika sheria, sera na taratibu. Tunatoa pia, katika baadhi ya matukio, usaidizi, msaada, au ushauri kwa wakimbizi binafsi, watafutaji hifadhi ya wakimbizi au watu wasio na taifa.

Mnamo Disemba 2016, sheria mpya inayoitwa **Kifungu cha Sheria cha Ulinzi wa Kimataifa 2015** ilianza kutekelezwa nchini Ayalandi. Ofisi ya UNHCR Ayalandi inaweka utaratibu mpya mmoja wa ulinzi wa kimatiafa kwa minajili ya kuchunguza maombi ya kupewa ulinzi wa kimataifa nchini Ayalandi. Kijitabu hiki cha taarifa kinatoa muhtasari wa mabadiliko makuu katika sheria mpya na mchakato mpya wa kupewa ulinzi kama mkimbizi na kinalenga kuwasaidia watu wanaotafuta ulinzi wa kimataifa nchini Ayalandi na wale wanaofanya kazi na watu wanaotuma maombi ya kupewa ulinzi.[1]

# Mashirika ya Kutoa Uamuzi

Haya ni mashirika yatakayochunguza ombi lako la kupewa ulinzi wa kimataifa.

### Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa (International Protection Office, IPO)

IPO, ambayo ni ofisi iliyo ndani ya shirika la Kiairishi la Kutoa Uraia wa Kuandikishwa na Huduma za Uhamiaji (Irish Naturalisation and Immigration Service, INIS), ndiyo iliyo na jukumu la kuchunguza maombi ya ulinzi wa kimataifa. Uhuru wa wahudumu wa IPO wanaotoa uamuzi kuhusu ulinzi wa kimataifa umelindwa katika sheria ya Kiairishi. Ili kudai hifadhi ya wakimbizi nchini Ayalandi, mbali na sehemu ya kiingilio, lazima utume ombi wewe binafsi kwa IPO. Ofisi ya IPO ilichukuanafasi ya Ofisi ya Kamishna wa Maombi ya Wakimbizi (Office of the Refugee Applications Commissioner, ORAC) mwanzoni mwa mwaka wa 2017. Ili kujua zaidi tafadhali nenda katika: **www.ipo.gov.ie**

### Mahakama ya Rufaa za Ulinzi wa Kimataifa (International Protection Appeals Tribunal, IPAT)

IPAT ni mahakama huru. Inachunguza rufaa za watu ambao IPO imependekeza kwamba wasipewe ulinzi wa kimataifa (hadhi ya wakimbizi au hifadhi mbadala) IPAT ilichukua nafasi ya Mahakama ya Rufaa za Wakimbizi (Refugee Appeals Tribunal, RAT) mwanzoni mwa mwaka wa 2017. Ili ujifahamishe mengi zaidi tafadhali nenda katika: **www.protectionappeals.ie**

[1] **Kanusho:** Kijitabu hiki ni kwa madhumuni ya taarifa pekee, hakijumuishi ushauri wa kisheria na kinaweza kubadilishwa. Kwa taarifa zaidi tafadhali tazama Kijitabu cha Maelezo kwa Waombaji wa Ulinzi wa Kimataifa **www.ipo.gov.ie**

# 1 Utaratibu Mmoja

Badiliko kubwa zaidi lililoanzishwa na kifungu cha sheria cha Ulinzi wa Kimataifa cha 2015 ni utaratibu mpya mmoja wa kuchunguza maombi ya ulinzi wa kimataifa. Hii inamaanisha kwamba hadhi ya wakimbizi, hifadhi mbadala na kibali cha kusalia vyote vitachunguzwa kwa pamoja katika mchakato mmoja. Hii inafaa kuzuia kucheleweshwa kwa utaratibu wa kutoa hifadhi kwa wakimbizi.

**Hadhi ya Wakimbizi** | **Hifadhi Mbadala** | **Kibali cha Kusalia**

**Utaratibu Mmoja**

# 2 Mchakato wa Utumaji Ombi

Mchoro huu unatoa muhtasari wa mchakato mpya wa utumaji ombi nchini Ayalandi na unafaa kusomwa pamoja na maandishi yaliyo hapa chini kwa kila hatua. Michoro ya maelekezo yenye maelezo inapatikana katika sehemu ya nyuma ya kipeperushi hiki cha taarifa.

**HATUA YA 1**
Ombi kwa Ofisi ya **Ulinzi wa Kimataifa**

**HATUA YA 2**
Mahojiano ya Mwanzo

**HATUA YA 3**
Hojaji

**HATUA YA 4**
Mahojiano ya Kibinafsi

**HATUA YA 5**
Uamuzi

Kama utafanikiwa utapokea

**Hadhi ya Mkimbizi, Hifadhi Mbadala**
au
**Kibali cha Kusalia**

**HATUA YA 6**
Kama hutafanikiwa kata rufaa kwa **Mahakama ya Rufaa za Ulinzi wa Kimataifa**

**HATUA YA 7**
Kama rufaa haitafanikiwa hakiki Uamuzi wa Kibali cha Kusalia

## **Hatua ya 1** Utumaji Ombi la Ulinzi wa Kimataifa

Unaweza kuomba ulinzi wa kimataifa kwenye mipaka ya Taifa au ukiwa tayari ndani ya Taifa kupitia IPO. Unaweza kuomba ulinzi wa kimataifa kwa niaba yako mwenyewe na/au kwa niaba ya watoto wako wanaokutegemea walio chini ya umri wa miaka 18. Kama watoto wako wamezaliwa ndani ya Taifa au wanaingia ndani yake wakati ukiwa katika utaratibu wa kupewa ulinzi, basi watakuwa wategemezi wako moja kwa moja katika ombi lako isipokuwa kama wao ni raia wa Ayalandi. Kama mtumaji ombi aliye na watoto ni muhimu sana kwamba ueleze malalamiko yoyote ya ulinzi yanayohusiana na watoto wako pamoja na wewe mwenyewe wakati wa utaratibu huu.

**Tusla, Wakala wa Mtoto na Familia,** inaweza kuomba ulinzi wa kimataifa kwa watoto ambao hawajaandamana na yeyote ili wawe katika utunzaji wao.

## **Hatua ya 2** Mahojiano ya Mwanzo

Kama utaomba ulinzi wa kimataifa katika mipaka ya Taifa, kama vile uwanja wa ndege au bandarini, ofisa wa uhamiaji na/au ofisa wa IPO wanaweza kukuhoji. Watafanya hivyo kwa madhumuni ya kukusanya taarifa ya mwanzo kama vile utambulisho wako, nchi yako ya asili, njia uliyosafiria hadi Ayalandi na misingi ya jumla unayoombea ulinzi wa kimataifa. Pale ambapo mahojiano haya ya mwanzo hayajafanyika katika mipaka ya Taifa, basi yatatekelezwa katika IPO.

Mahojiano ya mwanzo yatachunguza pia kama ombi lako linakubalika. Hii inamaanisha kwamba ofisa wa IPO ataamua kama unaweza kutuma ombi la hifadhi ya wakimbizi nchini Ayalandi. Huenda usiweze kufanya hivyo kama tayari umepewa hadhi ya mkimbizi au hifadhi mbadala katika Taifa jingine ambalo ni Mwanachama wa Umoja wa Ulaya, au kama kunayo nchi nyingine nje ya Umoja wa Ulaya ambayo imekupa hadhi ya mkimbizi na utaruhusiwa kurudi huko ambako utapewa ulinzi.

**Nini hufanyika kama ombi langu litapatikana kuwa halikubaliki?**

**Utapokea uamuzi wenye mantiki kutoka kwa IPO ambao utajumuisha kipimo cha muda cha kuwasilisha rufaa kwa IPAT. Rufaa ya IPAT itakuwa kwa maandishi pekee.**

Kama mahojiano yako ya mwanzo yalifanyika katika mipaka ya Taifa, utaelekezwa basi kwenye majengo ya IPO. Ukifikia kwenye IPO, wewe na wote wanaokutegemea mtachukuliwa alama za vidole na kufotolewa picha. Taarifa hii inachukuliwa kwa madhumuni ya utambuzi wa utambulisho wenu na kujua kama Sheria ya Dublin inaweza kutumika katika kesi yenu.

Kisha utaweza kupewa cheti cha muda cha makazi kinachoonyesha kwamba unayo ruhusa ya kuwa Ayalandi wakati ombi lako la ulinzi wa kimataifa likishughulikiwa. Hii si kadi rasmi ya utambulisho lakini unafaa kuwa nayo nyakati zote. Unaweza kupewa nyingine mpya wakati wa utaratibu wa ulinzi.

## **Hatua ya 3** Hojaji

Ofisa wa IPO atakupa kijitabu cha taarifa kuhusu utaratibu mmoja na hojaji ya kujaza na kurudisha kwa IPO. Ni muhimu sana kwamba ukisome kijitabu cha maelezo mapema kabla ya kuijaza hojaji na kuutafuta usaidizi wa kisheria.

Ni muhimu kwamba uijaze hojaji kabisa na utoe taarifa sahihi kuhusiana na mahitaji yako ya ulinzi wa kimatifa. Kama huelewi baadhi ya sehemu za hojaji, mwulize wakili wako kwa usaidizi.

Pale inapowezekana, hojaji inafaa kurudishwa ndani ya siku 20 za kufanya kazi yaani wiki 4. Hii ni kwa minajili ya kusaidia IPO katika kuchakata maombi kwa njia bora iwezekanavyo. Kama unahitaji muda zaidi wa kuijaza Hojaji au kushauriana na mshauri wa kisheria IPO imehakikishia watumaji ombi kwamba wataweza kuruhusiwa kufanya hivyo. Kama hili linakuhusu wewe, zungumza na wakili wako au wasiliana na IPO kwa njia ya moja kwa moja ili kuwajuza (Tazama ukurasa wa 21 kwa taarifa ya mwasiliani).

Ni muhimu kwamba uweze kuwasilisha pia stakabadhi zozote saidizi unazofikiria zitafaa katika ombi lako. Hizi zinajumuisha taarifa yoyote inayohusiana na ombi lako la kibali cha kusalia.

## **Hatua ya 4** Mahojiano ya Kibinafsi

IPO itakutumia barua ya miadi ya mahojiano yako. Mkalimani anaweza kuwepo kwa ajili yako, kama atahitajika. Kama unayo taarifa ya ziada na/au ushahidi tangu ulipoiwasilisha hojaji yako jaribu kuiwasilisha taarifa hii anagalau wiki moja mapema kabla ya mahojiano yaliyoratibiwa.
Mahojiano ni fursa yako ya kutoa sababu zote zinazoelezea kwa nini unatafuta ulinzi nchini Ayalandi. Siku ya mahojiano tafadhali angalia kama wewe na mkalimani mnaelewana.

Kama unao ugumu wowote wa kumwelewa mkalimani sema katika mahojiano yako na ofisa wa IPO. Ofisa wa IPO anayekuhoji atakuwa ameisoma mapema hojaji yako iliyojazwa na atakuwa ameielewa kesi yako. Kama unao ugumu wowote wa kuyaelewa maswali yanayoulizwa na ofisa wa IPO anayekuhoji tafadhali mwombe kurudia swali. Tafadhali kumbuka kwamba unalo jukumu la kusasisha Waziri kuhusu mabadiliko yoyote ya hali yanayohusu ombi lako la kibali cha kusalia mpaka pale ripoti itakapotayarishwa na Waziri kuhusiana na uamuzi huo wa kibali cha kusalia.

Kama ungependa kutoa taarifa ya ziada kuhusiana na swala la kibali cha kusalia katika ombi lako, hii ni fursa yako ya kufanya hivyo. Wewe au wakili wako mnaweza kutoa uwakilishi kwa maandishi kuhusiana na ombi lako mpaka na pamoja na siku ya mahojiano yako.

Rekodi iliyoandikwa ya mahojiano yako itahifadhiwa na ofisa wa IPO anayekuhoji. Kwa vipindi fulani wakati wa mahojiano, anayekuhoji atasita na kukuomba kuhakiki nakala za kile ulichosema na kufanya ufafanuzi wowote au masahihisho kama yatahitajika. Kisha utaombwa kupiga saini katika rekodi ya mahojiano ili kuthibitisha usahihi wake. Kama kutakuwa na lolote katika rekodi ya


mahojiano ambalo si sahihi, au kama kutakuwa na lolote lililoachwa, mfahamishe ofisa anayekuhoji kwa njia ya moja kwa moja ili uweze kulifafanua.

Wakili wako anaweza kuhudhuria mahojiano kama atapenda ingawa haya si mazoea kwa kawaida. Yeye anaweza pia kutoa uwakilishi kwa niaba yako kabla ya mahojiano. Kama wewe ni mtoto ambaye hajaandamana na yeyote, mlezi au mwakilishi wako kutoka Tusla lazima ayahudhurie mahojiano. Mahojiano yanaweza tu kuhahirishwa katika hali za kipekee, kwa mfano, wakati unaugua. Ni muhimu kwamba uifahamishe IPO mara moja kama huwezi kuyahudhuria mahojiano kwenye tarehe iliyo ratibiwa.  Mahojiano huenda yasitekelezwe lakini hilo si jambo la kawaida.[2]

## **Hatua ya 5** Uamuzi wa IPO

Baada ya mahojiano IPO itatilia maanani taarifa zote zinazohusiana na kesi yako. Hii inajumuisha rekodi ya mahojiano na hojaji iliyojazwa. Kama pendekezo halijatolewa ndani ya miezi sita unaweza kuomba taarifa ya muda uliyokadiriwa wa kupokea uamuzi kutoka kwa IPO.

Matokeo tofauti yanayoweza kutolewa juu ya ombi lako yamewekwa wazi katika jedwali hapa chini. Pendekezo litajumuisha kauli ya sababu za jinsi pendekezo lilifikiwa katika ombi lako la kibinafsi. Mambo fulani katika pendekezo yanaweza pia kuathiri kipimo cha muda kwa rufaa yoyote na kama kikao cha kujadili kesi yako kinaruhusiwa au la mbele ya IPAT.




[2] Kwa taarifa zaidi tazama sehemu ya 4.5.12 ya Kijitabu cha Maelezo kwa Waombaji wa Ulinzi wa Kimataifa.

Wewe na/au wakili wako mtapokea pendekezo kupitia barua iliyosajiliwa itakayotumwa kupitia posta. Kama IPO inapendekeza kwamba unafaa kupewa hadhi ya mkimbizi, Waziri wa Haki na Usawa (Waziri) atakutangaza rasmi kama i mkimbizi ndani ya wiki kadhaa. Katika hali finyu kabisa Waziri anaweza kukataa kufuata pendekezo la IPO wakati mtumaji ombi ataonekana kuwa ni hatari kwa usalama.

Kama utanyimwa hadhi ya mkimbizi lakini upewe hifadhi mbadala bado unayo haki ya kukata rufaa kwa IPAT ili kupata hadhi ya mkimbizi. Kama utakatazwa hadhi ya mkimbizi na hadhi ya hifadhi mbadala, Waziri ataamua kama atakupa "kibali cha kusalia au la". Kama uamuzi huo ni wa kukupa au kutokupa kibali cha kusalia, bado utakuwa na haki ya kukata rufaa kwa IPAT dhidi ya uamuzi wa kukunyima ulinzi wa kimataifa.

Kama utanyimwa hadhi ya mkimbizi na/au ile ya hifadhi mbadala, utapokea nakala ya rekodi ya mahojiano na kauli kuhusu haki yako ya kukata rufaa kwa Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa. Utapokea pia taarifa kuhusu utaratibu wa kufuatwa na fomu ya rufaa ya kuwasilisha rufaa kama hiyo. Kwa michoro yenye malezo zaidi kuhusu matokeo yanayoweza kutokea kuhusiana na ombi lako, tafadhali nenda katika sehemu ya nyuma ya kipeperushi hiki cha taarifa.

## Hatua ya 6 Kukata Rufaa kwa Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa

Unaweza kukata rufaa kwa IPAT dhidi ya pendekezo la IPO kwamba hustahili hadhi ya mkimbizi wala hifadhi mbadala. Huwezi kukataa rufaa kwa IPAT ikiwa umenyimwa kibali cha kusalia.

Fomu ya rufaa lazima ijazwe na kuwasilishwa kwa IPAT ndani ya vipimo vya muda vinavyofaa ambavyo utafahamishwa kuvihusu katika barua yako ya pendekezo ya IPO. Unaweza kuomba kikao cha kujadili kesi yako ya rufaa kulingana na matokeo yatakayotokana na barua yako ya pendekezo ya IPO.

Utafahamishwa wakati rufaa yako imepewa tarehe ya kusikizwa. Kwenye siku ya kikao, kama mkalimani atahitajika, tafadhali angalia kama wewe na mkalimani wako mnaelewana. Kama unao ugumu wowote wa kumwelewa mkalimani mweleze Mwanachama wa Mahakama. Kwenye kikao cha kujadili kesi yako, mwanachama wa IPO atahudhuria pamoja na wewe, wakili au mwanasheria wako pamoja na Mwanachama wa Mahakama. Mwanachama wa Mahakama anaweza pia kuelekeza mahudhurio ya shahidi mbele ya mahakama ili kutoa ushahidi kuhusiana na maswala fulani ya ombi lako la ulinzi.

IPAT ikitupilia mbali pendekezo hasi kutoka kwa IPO, Waziri atakupa tangazo linalofaa la ulinzi yaani hadhi ya mkimbizi au hifadhi mbadala.

**Je nikipokea kibali cha kusalia kutoka kwa IPO na ninataka kukata rufaa dhidi ya pendekezo la kunyimwa hadhi ya mkimbizi au hifadhi mbadala?**

**Kama utapewa kibali cha kusalia unaweza bado kukata rufaa dhidi ya pendekezo la IPO la kukunyima ulinzi wa kimataifa. Unaweza pia kusajili kibali chako cha kusalia katika ofisi yako ya usajili wa uhamiaji iliyo nchini mwako.**

## **Hatua ya 7** Uhakiki wa Kibali cha Kusalia

Kama Waziri hakukupa kibali cha kusalia, na rufaa yako kwa IPAT haikufaulu, Waziri atahakiki uamuzi wa kutokupa kibali cha kusalia pale ambapo umewasilisha taarifa yoyote mpya tangu uamuzi asilia ulipotolewa. Utapokea fomu ya uhakiki ya kibali cha kusalia ili uijaze. Utakuwa tu na **siku 5 za kufanya kazi** kabla ya kuwasilisha taarifa mpya hivyo basi hakikisha kwamba umetayarisha mapema stakabadhi zozote ambazo ungependa kuwasilisha. Ikiwa hali zako zitabadilika katika muda uliopo kati ya uamuzi wa Waziri wa kutoa kibali cha kusalia cha mwanzo na uamuzi wa IPAT kuihusu rufaa yako na unayo taarifa mpya ambazo ni muhimu kwa uhakiki wa kibali chako cha kusalia basi unafaa kumfahamisha Waziri haraka iwezekanavyo.

Waziri anaweza pia kutoa kibali cha kusalia kama kutofanya hivyo kutasababisha ukiukaji wa uzuiliwaji wa kurudishwa kwa lazima (kwa taarifa zaidi, tazama **7. Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara**).

# 3 Haki na Majukumu ya Watumaji Ombi

## HAKI ZANGU NI ZIPI ?

**Haki zako zinajumuisha:**

Kama wewe ni mtumaji ombi la ulinzi wa kimataifa haki zako zinajumuisha:

- Ruhusa ya kuingi na kusalia nchini Ayalandi kwa uchunguzi wa ombi lako la ulinzi wa kimataifa na IPO rufaa yoyote kwa IPAT
- Haki ya kupata ushauri wa kisheria na uwakilishi kutoka kwa wakili
- Haki ya kushughulikiwa kwa heshima, utu na haki kwenye utaratibu wote huu mmoja
- Haki ya kutoa mawasilisho ya kuandikwa kwa Waziri kuhusiana na ombi lako la ulinzi
- Matumizi ya mkalimani pale anapohitajika ili kuhakikisha mawasiliano
- Haki ya ufaragha
- Haki ya kufahamishwa kwa kuandikiwa kuhusu mahojiano yoyote, maamuzi au notisi nyingine muhimu kuhusiana na ombi lako la ulinzi wa kimataifa.
- Haki ya kuwasiliana na UNHCR

Usaidizi wa kisheria unapatikana kutoka katika **Bodi ya Usaidizi wa Kisheria (LAB)**. Bodi hiyo Itakupa mmojawapo wa wakili wake au wakili mwingine wa kibinafsi ambaye anafanya kazi na bodi hiyo. LAB imejitolea katika kuwapa wateja wote wa ulinzi wa kimataifa ushauri wa kisheria wa mapema kuhusu maswala yote ya ombi lao. Ushauri huo unaweza kujumuisha ushauri wa mwanzo kabla ya kuijaza hojaji yako na ushauri wa kabla ya mahojiano ambapo ushauri wa kisheria kuhusu maelezo mbalimbali ya madai yako kutokana na hojaji yako iliyojazwa utaweza kutolewa. **Kituo Huru cha Sheria cha Baraza la Kiarishi la Wakimbizi** kitatoa pia ushauri wa mapema wa kisheria kulingana na uwezo wake. Kama unazo fedha unaweza pia kutafuta huduma za wakili wako binafsi.

Kulingana na hali mbalimbali za kibinafsi za ombi lako unaweza kupendelea mkalimani wa jinsia fulani kuwepo wakati wa mahojiano au kikao cha rufaa. Ni muhimu kwamba ueleze suala hili mapema iwezekanavyo kwa IPO na/au IPAT ili waweze kutilia maanani ombi hili pale wanapoweza.

Taarifa yote iliyotolewa kuhusiana na ombi lako itashughulikiwa kwa ufaragha na haitafichuliwa kwa mamlaka ndani ya nchi yako ya asili / nchi yako ya makazi au kwa wawakilishi wa nchi yako ndani ya Ayalandi.

# MAJUKUMU YANGU NI YAPI?

### Majukumu yako yanajumuisha:

- Wajibu wa kutii sheria ndani ya Ayalandi

Hii inamaanisha lazima uheshimu sheria na masharti ya Ayalandi.

- Wajibu wa kushirikiana na mamlaka husika

Kama mtumaji ombi katika utaratibu mmoja unao wajibu amilifu wa kushirikiana na mamlaka husika katika uchunguzi wa ombi lako la ulinzi na katika uamuzi wa rufaa yoyote inayohusiana na ombi hilo. Lazima pia uwasilishe haraka iwezekanavyo taarifa yote inayohitajika kuthibitisha ombi lako na uwe muaminifu. Kukataa kushirikiana na mamlaka husika kunaweza kuwa na athari katika matokeo ya ombi lako la ulinzi.

### Majukumu ya kitaratibu

Sehemu ya wajibu wa kushirikiana na mamlaka husika inajumuisha majukumu yafuatayo:

a. Kutoondoka au kujaribu kuondoka nchini Ayalandi wakati wa utaratibu mmoja bila ya kibali cha Waziri;

b. Kufahamisha Waziri kuhusu anwani yako na badiliko lolote la anwani yako kwa kumuandikia barua haraka iwezekanavyo;

c. Kutii jukumu la kutoa ripoti zozote ambazo huenda ukahitajika kutoa kama vile hitaji la kuishi au kubakia katika mahali au sehemu bainishwa nchini Ayalandi na/au kujiwasilisha kwa ofisa wa uhamiaji baada ya muda uliyobanishwa au kijiwasilisha katika kituo bainishwa cha polisi (Garda);

d. Kuonyesha jina, anwani, uraia na nambari yako ya kitambulisho katika cheti chako cha makazi ya muda wakati unapokuwa na mawasiliano yoyote na IPO au IPAT;

e. Kuwa muaminifu katika ombi lako la ulinzi wa kimataifa na kuijaza hojaji yako kwa taarifa zinazofaa ili ombi lako liweze kuchunguzwa;

f. Kubakia na nakala zote za stakabadhi ulizopewa au zile ulizopea IPO na IPAT.

**Je, ninaweza kufanya kazi wakati ombi langu la ulinzi wa kimataifa linachunguzwa ?**

**Ikiwa hujapokea uamuzi kuhusu ombi lako la ulinzi kutoka kwa IPO ndani ya miezi 6, na hatua zako mwenyewe hazijasababisha kuchelewa huko, unaweza kutuma ombi la kibali cha kufanya kazi. Kwa maelezo zaidi angalia: www.inis.gov.ie**

# 4 Taarifa Nyingine Zinazofaa

### Kipaumbele

Aina fulani za maombi zinaweza kupewa kipaumbele na IPO. Hii inamaanisha kwamba maombi kama hayo yataratibiwa kwa mahojiano haraka iwezekanavyo. Hiyo haiamui mapema uamuzi utakaotolewa katika hali kama hizo au haitoi uhakikisho wowote wa ziada kuhusiana na ni lini uamuzi utafanywa katika hali kama hizo.

Kesi yako inaweza kupewa kipaumbele kwa sababu fulani, zikiwemo kama unao umri wa zaidi ya 70 (na kama wewe si sehemu ya kundi la familia), mtoto ambaye hajaandamana na yeyote, kwa sababu ya kuwa na matatizo mazito ya kiafya au kutokana na taifa unalotoka (Syria, Eritrea, Irak, Afganistani, Iran, Libya na Somalia).

IPO, kwa ushauriano na UNHCR, imetoa notisi kuhusu kupatia maombi ya aina fulani kipaumbele ambayo inaweza kupatikana katika: **http://www.ipo.gov.ie/en/ipo/pages/prioritisation_applicants**

### Kujiondoa

Uko huru kuondoa ombi lako la ulinzi au kukata rufaa wakati wowote kabla ya ripoti kutayarishwa kuhusiana na ombi lako na IPO au uamuzi kutolewa na IPAT. Ni muhimu kwamba utafute ushauri wa kisheria kabla ya kuliondoa ombi lako ili uelewe kabisa athari za kujiondoa kwako wewe na kwa yule/wale wanaokutegemea. Baada ya kujiondoa uchunguzi wa ombi lako utakamilishwa na Waziri atakataa kukupa hadhi ya mkimbizi au hifadhi mbadala.

### Kurud kwa hiari

Unalo chaguo la kurudi kwa hiari katika nchi yako ya asili /makazi katika hatua yoyote ya utaratibu mmoja. Ukiamua kurudi kwa hiari Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) linaweza kukupa usaidizi na ushauri, ukiwemo usaidizi wa kifedha kwa usafiri wako. Kitengo cha kurudi kwa hiari cha INIS kinaweza pia kukupa usaidizi.

Ili kupata kibali cha kurudi kwa hiari wakati wa mchakato, lazima uliondoe ombi lako la ulinzi wa kimataifa katika IPO au uiondoe rufaa yako katika IPAT. Waziri atakufahamisha pia kuhusu uwezekano wa kurudi kwa hiari katika nchi yako ya asili /makazi kufikia mwisho wa mchakato endapo hutapewa ulinzi wa kimataifa nchini Ayalandi na hutapewa kibali cha kusalia. Ili ujifahamishe mengi zaidi, tafadhali tembelea: **https://www.youtube.com/watch?v=eX7GarY2rUE**

### Sheria ya EU Dublin

Sheria ya EU Dublin ni zana ya kisheria ambayo inaamua ni Taifa lipi Mwanachama ambalo linalo jukumu la uchunguzi wa ombi la ulinzi wa kimataifa. Unapotoa ombi la ulinzi wa kimataifa IPO itakupa kipeperushi cha taarifa kuhusu Sheria ya EU Dublin. Ni muhimu kwamba ukisome kipeperushi hicho cha taarifa kwa makini kwani kunaweza kuwa na sababu zinazoelezea ni kwa nini taifa jingine mwanachama linalo jukumu la kushughulikia ombi lako, ikiwemo kama wanafamilia wako wapo katika Taifa jingine Mwanachama wa Umoja wa Ulaya. Kama ombi lako linapswa kushughulikiwa chini ya Sheria ya EU Dublin, utapokea kipeperushi kingine cha taarifa kuuhusu Sheria ya EU Dublin na athari zake kwa kesi yako binafsi.

### Ombi jingine la ulinzi wa kimataifa

Kama umekataliwa hadhi ya mkimbizi na hifadhi mbadala na ombi lako limefungwa, kibali cha Waziri kinahitajika kama utapenda kutuma ombi jingine la pili au la ziada kwa minajili ya ulinzi wa kimataifa nchini Ayalandi. Unweza kutuma ombi kwa kwa kumuandikia Waziri ukitafuta kibali cha ombi jingine. Mambo yatakayotiliwa maanani yanajumuisha yafuatayo:

a. Tangu uwasilishe ombi lako la hapo awali, huenda kuna taarifa mpya ambazo zitafanya kuwe na uwezekano mkubwa zaidi kwamba utahitimu kupata ulinzi wa kimataifa na kwamba hukuweza kutoa taarifa hizo a mapema zaidi katika ombi la awali;

b. Kama ombi lako la awali liliondolewa au lilionekana kuondolewa wakati hukuweza kulikamilisha kwa sababu ambazo hukuweza kuziepuka.

Kama Waziri atakataa kukupa kibali cha ombi lingine la ulinzi wa kimataifa, utapewa uamuzi wenye mantiki kuhusu kwa nini amefanya hivyo na unaweza kuukatia rufaa katika IPAT.

### Uhakiki wa mahakama

Uhakiki wa kimahakama ni njia ya Mahakama Kuu kusimamia mashirika ya uendeshaji na Mahakama i, ikiwemo IPO na IPAT, ili kuhakikisha kwamba wanatoa uamuzi kwa njia sahihi na kulingana na sheria. Uhakiki wa mahakama si rufaa. Uhakiki wa mahakama unamruhusu mtumaji ombi, kwa ushauriano na wakili wake, kutafuta uamuzi wa IPO na/au IPAT kuhakikiwa kimahakama na Mahakama Kuu kulingana na sheria ya usimamizi ya Kiairishi, kwa mfano pale ambapo kumekuwa na kosa la sheria katika mchakato wa uamuzi unaohusu ombi lake. Wakili wako atakushauri kuhusu kama hali hiyo inaweza kutumika katika ombi lako. Ni muhimu kukumbuka kwamba Mahakama inayofanya uhakiki wa kimahakama haiwezi kupendekeza uamuzi mzuri kuhusiana na ulinzi wa kimataifa lakini itahitaji

IPO au IPAT kutoa uamuzi mpya ikizingatia matokeo ya kisheria ya Mahakama. Taratibu za uhakiki wa kimahakama zinaweza pia kuchukuliwa dhidi ya Waziri wa Haki na Usawa. Tafadhali ongea na wakili wako ili kuamua kama mojawapo ya machaguo haya yanafaa kutiliwa maanani katika kesi yako.

### Kuzuiliwa

Watumaji ombi kwa ujumla hawazuiliwi wakati wa utaratibu wa ulinzi nchini Ayalandi. Hata hivyo, katika hali fulani mtumaji ombi anaweza kukamatwa bila ya idhini na ofisa wa uhamiaji au mwanachama wa polisi (Garda Síochána) kama watakuwa na sababu nzuri za kushuku kwamba wewe mtumaji ombi:

I. ni tishio kwa usalama wa umma au kwa utulivu wa umma katika Taifa husika;

II. umetenda uhalifu mbaya usio wa kisiasa nje ya nchi ya Ayalandi;

III. hujafanya jitihada mwafaka katika kuweka wazi utambulisho wako;

IV. unanuia kuondoka nchini Ayalandi na bila ya mamlaka ya kisheria kuweza kuingia katika nchi nyingine;

V. umetenda au unanuia kutenda vitendo vitakavyokuwa na athari hasi kwa mfumo wa kuwapa watu ulinzi wa kimataifa katika Taifa husika, au kwa mpangilio wowote unaohusiana na Eneo Jumla la Usafiri, au

VI. bila ya sababu nzuri, umeharibu utambulisho wako au stakabadhi yako ya kusafiria, au umekuwa ukimiliki stakabadhi ya utambulisho ambayo ni ghushi, iliyobadilishwa au ni ya mtu mwingine.

Mtumaji ombi aliyekamatwa katika hali hizi anaweza kukamatwa na kuzuiliwa katika sehemu zilizobainishwa kwa lengo hilo kisheria. Watoto, ambao wanafafanuliwa kama mtu yeyote aliye na umri wa chini ya miaka 18, hawawezi kuzuiliwa chini ya sheria hii.

**Je, ninaweza kutuma ombi la ulinzi wa kimataifa kama nimekamatwa na polisi au nimo kizuizini?**

**Unaweza kutuma ombi la ulinzi wa kimataifa kama umekamatwa na polisi au umo kizuizini. Unafaa kumfahamisha Gavana wa jela au Garda katika kituo cha polisi ambapo umezuiliwa haraka iwezekanavyo kama ungependa kutuma ombi. Kesi yako itapewa kipaumbele kama utabakia kizuizini wakati wa uchunguzi wa ombi lako.**

**Je, kuzuiliwa kwangu kutahakikiwa na Mahakama?**

**Kama utazuiliwa kwa misingi iliyoelezwa hapo juu, utaletwa mbele ya jaji wa Mahakama ya Wilaya katika eneo ambayo umezuiliwa haraka iwezekanavyo. Jaji wa Mahakama ya Wilaya atahakiki matumizi ya kuzuiliwa kulingana na hali za kibinafsi za kesi yako.**

# 5 Wafadhiliwa wa Ulinzi wa Kimataifa:

### Faida zangu kama mfadhiliwa wa ulinzi wa kimataifa

Kama utapewa hadhi ya mkimbizi au hifadhi mbadala utastahili:

- Ruhusa ya kuishi nchini Ayalandi kwa kipindi bainishwa kisichopungua miaka 3;
- Kutafuta na kupata ajira, kujihusisha katika biashara, uuzaji na ununuzi au taaluma yoyote;
- Ufikivu wa elimu na mafunzo kwa njia sawa na raia wa Kiairishi;
- Kupokea utunzaji wa kimatibabu na faida za hali njema ya kijamii sawa na raia wa Kiairishi;
- Kupata haki sawa za usafiri kuelekea au kutoka nchini Ayalandi sawa na zile ambazo raia wa Kiairishi hupata (hata hivyo, tafadhali kumbuka huenda bado ukahitaji visa kuingia katika nchi nyingine);
- Tuma ombi kwa Waziri, ndani ya mwaka mmoja wa kupewa hadhi ya mkimbizi au hifadhi mbadala, ili upate ruhusa ya wanafamilia fulani wa familia yako kuweza kuingia na kuishi nchini Ayalandi pamoja nawe.

### Je, ninawezaje kutuma ombi la stakabadhi ya kusafiria ?

**Unaweza kutuma ombi kwa Waziri ili kupata stakabadhi ya kusafiria kwa kuijaza fomu ya ombi. Malipo ya ada ya €80 yanahitajika pia. Waziri hatatoa stakabadhi ya kusafiria kama mtu anayetuma ombi bado hajatoa taarifa inayohitajika katika kuchakata ombi hilo, mtu huyo anayetuma ombi anao hifadhi mbadala na anaweza kupokea pasipoti ya kitaifa au Waziri anafikiria kuwa kutoa stakabadhi hiyo ya kusafiria itakuwa ni hatari kwa usalama wa kitaifa, usalama wa umma, afya ya umma au utulivu wa umma au itakuwa kinyume cha sera ya umma.**

### Ninacho kibali cha kusalia. Je, ninaweza kutuma ombi la stakabadhi ya kusafiria?

**Kama hujapewa hadhi ya mkimbizi au hadhi ya hifadhi mbadala lakini umepewa kibali cha kusalia nchini Ayalandi, unafaa kutuma ombi la pasipoti kwa ubalozi wa nchi yako. Katika kesi fulani za kipekee watu ambao wamepewa kibali cha kusalia na ambao hawana pasipoti wanaweza kupewa stakabadhi mbadala ya kusafiria na Waziri wa Haki na Usawa.**

Haki za wakimbizi na wafadhiliwa wa hifadhi mbadala kwa ujumla ni sawa isipokuwa kama mkimbizi unastahili kuwa na stakabadhi ya kusafiria ya mkimbizi. Mfadhiliwa wa hifadhi mbadala atapokea tu stakabadhi ya kusafiria kutoka kwa INIS pale ambapo mtu huyo hawezi kupata pasipoti ya kitaifa kutoka katika nchi yake ya asili. Hadhi ya mkimbizi ni hadhi pia inayotambulika kimataifa kulingana na Mkutano wa Wakimbizi wa UN 1951 pamoja na Itifaki yake. Wakimbizi wanaweza pia kutuma ombi la Uraia wa Kiairishi baada ya miaka hii mitatu ilhali wafadhiliwa wa hifadhi mbadala lazima wasubiri miaka mitano.

Kama hutapewa hadhi ya mkimbizi na hifadhi mbadala lakini upewe kibali cha kusalia, kibali hicho kitakuwa kulingana na Sehemu ya 4 ya Kifungu cha Sheria ya Uhamiaji ya 2004. Ruhusa itakayotolewa inaweza kutegemea masharti fulani. Masharti hayo yanajumuisha urefu wa muda ambao ruhusa hiyo imetolewa na kama unaruhusiwa kuajiriwa,, kufanya biashara au kufanya taaluma yoyote katika Taifa husika. Kibali cha kusalia kinaweza kutolewa upya wakati itakapoisha, hata hivyo, urefu wa muda na masharti yaliyowekwa katika kibali hicho yanaweza kuhakikiwa wakati wowote.

Mtu aliyepewa kibali cha kusalia hana haki ya kuungana tena na familia kulingana na Kifungu cha Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa. Mtu huyo anaweza kutuma ombi la kuungana tena na familia yake kupitia kwa taratibu za kawaida za uhamiaji, hata hivyo, vigezo na maswala tofauti yatatumika.

### Kuungana tena na familia

Kama utapewa hadhi ya mkimbizi au hifadhi mbadala unaweza kutuma ombi ndani ya miezi 12 ya baada ya kupokea hadhi hiyo, kwa Waziri ili kupata ruhusa ya wanafamilia fulani katika familia yako kuingia na kuishi nchini Ayalandi pamoja nawe, au kama tayari wamo nchini Ayalandi, kuishi na kubakia hapo na wewe.

Kufuatia uchunguzi na uamuzi wa Waziri, mwanafamilia ataweza kupewa ruhusa ya kuishi nchini Ayalandi kwa kipindi fulani bainishwa kisichopungua mwaka 1, na ikiwa ruhusa hiyo inatolewa upya, kipindi kisichopungua miaka 2.

**Nani anayefafanuliwa kama mwanafamilia kwa madhumuni ya kuungana tena na familia?**

**Kama wewe ni mtumaji ombi mtu mzima, wanafamilia wako wanafafanuliwa kama (i) mume au mke wako au mume au mke wa ndoa ya kiraia, mradi tu ndoa hiyo ya kiraia ilikuwa halali wakati ulipotuma ombi la ulinzi wa kimataifa; (ii) mtoto wako, mradi tu awe chini ya umri wa miaka 18 na awe hajaoa wala kuolewa wakati ulipotuma ombi la ulinzi wa kimataifa.**

**Mimi ni mtoto ambaye hajaandamana na yeyote. Nani anafafanuliwa kama mwanafamilia wangu kwa madhumuni ya kuungana tena na familia?**

**Mzazi wako na kaka na dada zako mradi tu wawe chini ya umri wa miaka 18 au ambao hawajaoa wala kuolewa. Familia yako inafafanuliwa kuanzia wakati ule unapotuma ombi la kuungana tena na familia.**

## Ninawezaje kutuma ombi la kuungana tena na familia?

**Unaweza kutuma ombi la kuungana tena na familia, baada ya kupewa hadhi la mkimbizi au hifadhi mbadala, kwa kuandika barua kwa Kitengo cha Kuungana Tena na Familia, Huduma ya Kiarishi ya Uraia wa Kuandikishwa na Uhamiajia (Family Reunification Unit, the Irish Naturalisation and Immigration Service), 13/14 Burgh Quay, Dublin 2.**

### Utaratibu wa kutuma ombi la kuungana tena na familia

Lazima utume ombi la kuungana tena na familia ndani ya miezi 12 baada ya kuipokea hadhi ya mkimbizi au hadhi ya hifadhi mbadala kutoka kwa Waziri. Kwa mfano, kama ulipewa hadhi ya mkimbizi mnamo tarehe Machi 1 2017, lazima utume ombi la kuungana tena na familia kabla ya Machi 1 2018.

Lazima utume ombi kwa kuandika barua kwa kwa Kitengo cha Kuungana Tena na Familia, INIS na utoe taarifa ifuatayo:

- Jina lako, nambari yako binafsi ya kitambulisho na anwani;
- Tarehe ambayo ulipewa hadhi ya mkimbizi au hifadhi mbadala na Waziri;
- Kwa kila mwanafamilia: jina lake, uhusiano wake na wewe, tarehe yao ya kuzaliwa, uraia na anwani ya sasa.

Inaweza pia kuwa muhimu kutoa nakala ya barua yako ya kupewa hadhi ya mkimbizi au hifadhi mbadala katika mawasiliano yako. Baada ya ombi hili utapokea hojaji kutoka kwa Kitengo cha Kuungana Tena na Familia ili uijaze. Katika awamu hii, utaombwa pia kuwasilisha stakabadhi asilia zinazohusu wanafamilia wako kama vile vyeti vyao vya kuzaliwa, kadi za kitaifa za utambulisho na pasipoti pamoja na picha mbili za pasipoti za rangi zilizopigwa saini na za hivi karibuni. Unaweza pia kuhitajika kutoa stakabadhi yako ya kusafiria na ushahidi wa stakabadhi kuhusiana na anwani yako ya sasa. Kulingana na hali zako binafsi, unaweza pia kulazimika kuwasilisha cheti chako cha ndoa kama unatafuta kuungana tena na mume au mke wako au utoe taarifa nyingine muhimu au ushahidi wa stakabadhi.

Baada ya kuijaza na kuiwasilisha hojaji yako, Kitengo cha Kuunganisha Tena Familia kitaichunguza ombi lako na utapokea barua ya uamuzi. Kama kuungana tena na familia yako kutaidhinishwa utapokea barua ya uamuzi inayokupa ruhusa, tarehe ambayo mwanafamilia/wanafamilia wako lazima aingie na/au kuishi katika Taifa husika. Ni muhimu kwamba upange usafiri wao kabla ya tarehe hiyo kwani kama mwanafamilia/wanafamilia wako hataingia nchini Ayalandi kabla au katika tarehe hiyo, basi ruhusa hiyo ya kuungana tena na familia itabatilishwa.

## Mimi ni mwanafamilia ambaye amepokea hivi majuzi idhini ya kujiunga na mwanafamilia wangu nchini Ayalandi. Haki zangu ni zipi?

**Unayo ruhusa ya kuingia na/au kuishi nchini Ayalandi kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja, na endapo utajiandikisha upya, kwa kipindi kisichopungua miaka miwili. Kama mwanafamilia, unazo haki sawa na unastahili kila kitu ambacho mfadhili wako anapata, mradi tu ulinzi wa kimataifa wa mfadhili wako uwe ni halali na wewe huwe ni mkazi wa Taifa husika.**

# 6 Masharti ya Mpito

Baadhi ya watu watakuwa wametuma ombi la ulinzi wa kimataifa kabla ya kuanza kutekelezwa kwa Kifungu cha Sheria cha Ulinzi wa Kimataifa cha Disemba 31 2016. Mipangilio fulani imeweza kuwekwa ili kuhamisha maombi yao ya hadhi ya mkimbizi na hifadhi mbadala kutoka kwenye Ofisi ya Kamishna wa Maombi ya Wakimbizi (ORAC) na rufaa fulani kutoka kwenye Mahakama ya Rufaa za Wakimbizi (RAT) hadi kwenye ofisi mpya ya IPO. Watumaji ombi hao wanapaswa kuwa wamepokea barua binafsi kutoka katika IPO ikiwaelezea mipango ya uhamisho wa maombi yao.

Michoro hii iliyo hapa chini inaonyesha kategoria kuu za kesi zilizohamishwa hadi katika IPO. Ni muhimu kukumbuka kwamba vijisanduku vilivyo katika upande wa kushoto vinaonyesha maombi yaliyowasilishwa kabla ya Disemba 31 2016. Taarifa zaidi zinapatikana katika **nakala ya IPO ya taarifa kuhusu mipangili ya kimpito:** http://ipo.gov.ie/en/IPO/Pages/Transitional_Arrangements Tafadhali wasiliana na wakili wako kama unahitaji ushauri zaidi kuhusiana na ombi lako.

| | |
|---|---|
| **Nilituma ombi la hadhi ya mkimbizi katika ORAC kabla ya Disemba 31 2016 na bado sijapokea pendekezo la kesi yangu** | **Faili yako itahamishwa hadi katika IPO ili kuyachunguza mahitaji yako ya ulinzi wa kimataifa. Hii inamaanisha kwamba utaijaza hojaji mpya na kuwa na mahojiano mapya ndani ya utaratibu mmoja.** |
| **Ombi langu la hadhi ya mkimbizi lilikuwa limekatiwa rufaa katika RAT kabla ya Disemba 31 2016 lakini bado sijaupokea uamuzi wa Mahakama** | **Faili yako itahamishwa katika IPO ili ikaguliwe kwa ajili ya haki yako ya kupewa hifadhi mbadala pekee. Utakuwa na mahojiano mapya kuhusu hifadhi mbadala pekee. Kama IPO itakataa ombi lako la hifadhi mbadala basi Waziri atafikiria kama unafaa kupewa kibali cha kusalia. Kama utakata rufaa dhidi ya uamuzi wa kukatazwa hifadhi mbadala, rufaa yako itajumuisha rufaa ya haki ya kupewa hadhi ya mkimbizi ambayo ilihifadhiwa ili rufaa zote mbili ziweze kukaguliwa kwa pamoja yaani hadhi ya mkimbizi na hifadhi mbadala.** |
| **Nilituma ombi la hifadhi mbadala katika ORAC kabla ya Disemba 31 2016 lakini uchunguzi wa ombi langu bado haujaanza.** | **Faili yako itahamishwa katika IPO ili ikaguliwe kwa ajili ya haki yako ya kupewa hifadhi mbadala pekee. Utakuwa pia na hojaji na mahojiano mapya kuhusu hifadhi mbadala pekee. Pendekezo linalokukataza hadhi ya mkimbizi kwa mujibu wa ORAC na uamuzi wa RAT (kama litatumika) litabakia. Kama IPO itakataa ombi lako la hifadhi mbadala basi Waziri atafikiria kama unafaa kupewa kibali cha kusalia. Unaweza pia kukata rufaa kwa IPAT dhidi ya uamuzi wa kukukataza hifadhi mbadala uliyoafikiwa na IPO.** |

Ombi langu la hifadhi mbadala lilikuwa limekatiwa rufaa kwa RAT kabla ya Disemba 31 2016. Ombi langu litakuwaje?

IPAT, ambayo ilichukua nafasi ya RAT, itatoa uamuzi kuhusu rufaa ya hifadhi mbadala pekee. Kisha utakuwa na haki ya kutuma ombi kwa kumuandikia Waziri wa Haki na Usawa kuhusu "ruhusa ya kusalia" kulingana na Sehemu ya 3 ya Kifungu cha Sheria ya Uhamiaji 1999. Msingi wa uamuzi kama huo hutofautiana kwa kiasi fulani na maswala yanayozingatiwa kuhusiana na "kibali cha kusalia" yaliyotajwa katika Kifungu cha Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa 2015. Kwa taarifa zaidi tafadhali ongea na mwakilisi wako wa kisheria.

Niliwasilisha rufaa kwa RAT katika uamuzi unaohusiana na Sheria ya Dublin kabla ya Disemba 31 2016. Ombi langu litakuwaje?

IPAT, ambayo ilichukua nafasi ya RAT, itatoa uamuzi kuhusu rufaa ya Sheria ya Dublin pekee. Kama rufaa yako itafanikiwa basi ombi lako litakaguliwa nchini Ayalandi kupitia kwa taratibu za kawaida.

# 7 Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara:

**S** Ulinzi wa kimataifa ni nini?

**J** Ulinzi wa kimataifa ni kauli inayotumika mara kwa mara katika sheria ya Umoja wa Ulaya ambayo inamaanisha ulinzi wa watu wenye hadhi ya wakimbizi na wale wenye hadhi ya hifadhi mbadala. Mtu anayeomba hifadhi ya ukimbizi nchini Ayalandi anatafuta ulinzi wa kimataifa dhidi ya kushtakiwa au kupata madhara mabaya katika nchi yake ya asili.

**S** Mkimbizi ni nani?

**J** Mkimbizi ni mtu ambaye hawezi kurudi katika nchi yake kwa sababu ana hofu inayoeleweka kabisa ya kuteswa kwa sababu ya rangi, dini, uraia, uanachama katika kundi fulani la kijamii au maoni ya kisiasa.

Hadhi ya mkimbizi ni mfumo wa ulinzi unaotolewa kwa watu ambao wamehitimu kufafanuliwa kama wakimbizi.

**S** Hifadhi mbadala ni nini?

**J** Hifadhi mbadala unaenda sambamba na hadhi ya mkimbizi. Unamaanisha kwamba mtu haweza kurudishwa katika nchi yake ya asili au ya makazi kwa sababu anakabiliwa na hatari halisia ya madhara makali. Madhara makali yanamaanisha (i) adhabu ya kifo au kufungwa jela; (ii) mateso au kutendewa vitendo vya kinyama au vya kudhalilisha au adhabu; (iii) tishio kali na la kibinafsi kwa maisha ya raia au mtu kupitia vitendo vya aina mbalimbali vya ukatili katika hali ya vita vya kimataifa au vya ndani kwa ndani vya kutumia silaha.

**S** Kibali cha kusalia ni nini?

**J** Kibali cha kusalia kitachunguzwa tu kama utapatikana kuwa hustahili hadhi ya mkimbizi au hifadhi mbadala. Hapa ndipo Waziri atafikiria kama atakupa kibali cha kusalia nchini Ayalandi kwa sababu nyingine kama vile hali zako binafsi au za familia.

Waziri atazingatia mambo kama vile:

a. asili ya uhusiano wako na nchi ya Ayalandi, kama ipo;
b. maswala ya kibinadamu;
c. hulka na mwenendo wako nchini Ayalandi na kwingineko, pamoja na kama umewahi kushtakiwa kwa uhalifu wowote;
d. Faida za jumla zinazoweza kupatikana.

Wakati anafikiria kukupatia kibali cha kusalia, Waziri atazingatia pia uzuiliwaji wa kurudishwa nyumbani kwa lazima.

**S** Kuzuiliwa kurudishwa nyumbani kwa lazima kunamaamisha nini?

**J** Kanuni hii inamaanisha kwamba Waziri hawezi kumtimua au kumrudisha mtu yeyote, kwa njia yoyote ile kwenye mpaka wa eneo ambapo, kwa maoni ya Waziri (a) maisha au uhuru wa mtu huyo utatishiwa kwa sababu za rangi, dini, uraia, uwanachama wa kundi fulani la kijamii au maoni ya kisiasa (b) kunayo hatari kuu ambapo mtu huyo atapewa adhabu ya kifo, mateso au vitendo vingine vya kinyama au vya kudhadhilisha au adhabu.

**S** "Ruhusa ya kusalia" ni nini?

**J** Ruhusa ya kusalia inamaanisha utaratibu ambao ulikuwepo kabla ya Kifungu cha Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa 2015 kuanza kutekelezwa. Sehemu ya 3 ya Kifungu cha Sheria ya Uhamiaji ya 1999 inaweka wazi mambo ambayo Waziri atazingatia katika kufikia uamuzi wa kutoa ruhusa ya kusalia. Masharti husika yanaendelea kutumika katika kesi za watu ambao kurudishwa kwao nyumbani kwa lazima kunafikiriwa na ambao hajawahi kutuma ombi la hifadhi ya wakimbizi. Idadi ndogo ya kesi za mpito (tazama hapo juu) zitaendelea kushughulikiwa kupitia kwa taratibu hizi.

**S** Inamaanisha nini kutegemea ombi la ulinzi wa kimataifa la mzazi?

**J** Inamaanisha kwamba ukaguzi wa ombi la ulinzi wa kimataifa la mtoto anayetegemea mzazi utajumuishwa katika ukaguzi wa ombi la mzazi wake na unaweza kutegemea matokeo ya

ombi hilo la mzazi. Mtoto anayetegemea mzazi hatakuwa na mahojiano yake binafsi au uchunguzi wake binafsi wa mahitaji yake ya ulinzi. Mzazi anafaa kujumuisha sababu zozote katika mchakato wake wa kutuma ombi kuhusu ni kwa nini mtoto huyo anahitaji ulinzi wa kimataifa na/au ni kwa nini anafaa kupewa kibali cha kusalia nchini Ayalandi. Ni muhimu kukumbuka kwamba watoto wanaweza kuwa na mahitaji ya ulinzi ya ziada au yaliyo tofauti na yale ya wazazi wao.

**S** Je, ninaweza kutuma ombi la ulinzi wa kimataifa nchini Ayalandi kama sina taifa?

**J** Ndiyo, unaweza kutuma ombi la hadhi ya mkimbizi na hifadhi mbadala nchini Ayalandi kama huna taifa. Kisha ombi lako litachunguzwa kuhusiana na nchi yako ya makazi yaani nchi uliyoishi hapo awali.

**S** Je kama ninao ulemavu na/au mahitaji mengine maalum?

**J** Unafaa kuifahamisha IPO haraka iwezekanavyo kuhusu ulemavu wowote au mahitaji mengine maalum ambayo unaweza kuwa nayo kwa ajili ya mahojiano yako ya kibinafsi ili IPO, pale inapoweza, iweze kutilia maanani mahitaji yako.


**S** Je, hadhi yangu ya mkimbizi au ya hifadhi mbadala inaweza kubatilishwa?

**J** Ndiyo, hadhi yako ya mkimbizi auya hifadhi mbadala inaweza kubatilishwa katika hali fulani finyu kama vile pale ambapo umepatikana kuwa ulitoa taarifa ya uwongo au potoshi wakati wa uchunguzi wa ombi lako la ulinzi wa kimatifa. Kama hali hiyo itafanyika basi utatumiwa notisi ya kuandikwa, kulihusu pendekezo la Waziri la kubatilisha hadhi yako, zikiwemo sababu zozote zilizosababisha ubatilishaji huo. Utapewa fursa ya kutoa malalamishi yako dhidi ya uamuzi huo kwa kumuandikia Waziri ndani ya siku 15 za kufanya kazi baada ya kupokea notisi hiyo. Baada ya Waziri kuamua kuibatilisha hadhi yako unaweza, ndani ya siku 10 za kufanya kazi kukata rufaa kwa Mahakama Husika dhidi ya uamuzi huo.


**S** Nitaishi wapi wakati wa utaratibu wa ulinzi wa kimataifa?

**J** Utapewa makazi na Wakala wa Mapokezi na Uwiano katika Kituo cha Kutoa Huduma Moja kwa Moja, hata hivyo, kama utakuwa na mbinu zako za kibinafsi za kifedha za kujitafutia makazi, unaweza kuishi kwingineko. Mfumo wa Mapokezi unasimamiwa na S.I. Nambari 230 ya 2018 ya Sheria za Jamii za Ulaya (Masharti ya Mapokezi) za 2018.

## UTOAJI WA HADHI YA MKIMBIZI KATIKA TUKIO LA 1





## UTOAJI WA HADHI YA MKIMBIZI KATIKA TUKIO LA 1



## UTOAJI WA KIBALI CHA KUSALIA KATIKA TUKIO LA 1



## KUKATAZWA HADHI YA MKIMBIZI, HIFADHI MBADALA NA KIBALI CHA KUSALIA KATIKA TUKIO LA 1



# 8 MAELEZO YA MWASILIANI YA MASHIRIKA MUHIMU

**Bado ungali na maswali kuhusiana na utaratibu mmoja mpya au Kifungu cha Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa baada ya kusoma kipeperushi hiki?**

Unaweza kuwasiliana na ofisi yetu na/au kumwuliza wakili wako.

**Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa Uraia wa Kuandikishwa wa Kiairishi & Huduma ya Uhamiaji (International Protection Office Irish Naturalisation & Immigration Service)**
79-83 Lower Mount Street,
Dublin 2, D02 ND99
**Simu:** +353 1 602 8000
**Faksi:** +353 1 602 8122
**Baruapepe:** ipo@justice.ie
www.ipo.gov.ie

**Ulinzi wa Kimataifa Mahakama ya Rufaa (International Protection Appeals Tribunal)**
6/7 Hanover Street,
Dublin 2, D02 W320
**Simu:** +353 1 474 8400
**Lo-Call:** 1890 210 458
**Faksi:** +353 1 474 8410
**Baruapepe:** info@protectionappeals.ie
www.protectionappeals.ie

**Uraia wa Kuandikishwa wa Kiairishi & Huduma ya Uhamiaji (Irish Naturalisation & Immigration Service)**
Department of Justice & Equality
13-14 Burgh Quay,
Dublin 2, D02 XK70
**Simu:** +353 1 616 7700
**Lo-Call:** 1890 551 500
www.inis.gov.ie

**Wakala wa Mapokezi na Uwiano (Reception and Integration Agency)**
P.O. Box 11487, Dublin 2
**Simu:** +353 1 418 3200
**Faksi:** +353 1 418 3271
**Baruapepe:** RIA_Inbox@justice.ie
www.ria.gov.ie

**Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (International Organisation for Migration)**
116 Lower Baggot Street,
Dublin 2, D02 R252
**Simu:** +353 1 676 0655
**Simu bila malipo:** 1800 406 406
**Baruapepe:** iomdublin@iom.int
www.ireland.iom.int

**Legal Aid Board Dublin**
48/49 North Brunswick Street,
Georges Lane, Dublin 7
D07 PE0C
**Simu:** +353 1 646 9600
**Faksi:** +353 1 671 0200
**Baruapepe:** lawcentresmithfield@legalaidboard.ie

**Legal Aid Board Galway**
9 Francis Street Galway,
H91 NS53
**Simu:** +353 91 561 650
**Faksi:** +353 91 563 825
**Baruapepe:** galwaylawcentre@legalaidboard.ie

**Legal Aid Board Cork**
Popes Quay Law Centre,
North Quay House,
Popes Quay, Shandon,
Cork, T23 HV26
**Simu:** +353 21 4551 686
**Faksi:** +353 21 455 1690
**Baruapepe:** lawcentrecorknorth@legalaidboard.ie

**Timu ya Watoto Waliotenganishwa Wanaotafuta Hifadhi ya Wakimbizi, Tusla - Wakala wa Mtoto & Familia (Team for Separated Children Seeking Asylum Tusla – Child & Family Agency)**
Sir Patrick Dun's Hospital,
Lower Grand Canal Street,
Dublin 2, D02 P667
**Simu:** +353 1 647 7000
**Faksi:** +353 1 647 7008
www.tusla.ie

**Baraza la Wakimbizi la Kiairishi (Irish Refugee Council)**
37 Killarney Street,
Mountjoy, Dublin 1
**Simu:** +353 1 764 854
**Faksi:** +353 1 672 5927
**Baruapepe:** info@irishrefugeecouncil.ie
www.irishrefugeecouncil.ie

**Nasc Ireland**
Ferry Lane, Dominic Street, Cork
**Simu:** +353 21 450 3462
**Baruapepe:** info@nascireland.org
www.nascireland.org

**Doras Luimni**
Central Buildings 51a,
O' Connell Street,
Limerick, V94 268W
**Simu:** +353 61 310 328
**Baruapepe:** info@dorasluimni.org
www.dorasluimni.org

**Crosscare Refugee Service**
2 Sackville Place, Dublin 1
**Simu:** +353 1 873 2844
**Faksi:** +353 1 872 7003
**Baruapepe:**
refugeeservice@crosscare.ie
www.crosscare.ie

**SPIRASI**
213 North Circular Road,
Phibsborough, Dublin 7
**Simu:** +353 1 838 9664
au +353 1 868 3504
**Faksi:** +353 1 882 3547
**Baruapepe:** info@spirasi.ie
www.spirasi.ie

**Jesuit Refugee Service Ireland**
The Mews, 20 Upper Gardiner St.
Dublin 1.
**Simu:** +353 1 814 8644
www.jrs.ie

**UNHCR**
102 Pembroke Road,
Ballsbridge, Dublin 4,
Ireland.
**Simu:** + 353 1 6314510
**Baruapepe:** iredu@unhcr.org
www.unhcr.ie

www.unhcr.ie

UNHCR
The UN Refugee Agency